



## TANZANIA NA ITALIA ZASAINI MKATABA WA SHILINGI BILIONI MOJA KUSADIA USAJILI WATOTO MKOA WA TANGA

### RITA - HABARI

Serikali ya Tanzania na Italia zimetiliana saini mkataba wa msaada wa Euro laki nne na elfu kumi sawa na takribani shilingi bilioni moja kwa ajili ya programu ya kuimarisha mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu hapa nchini.

Msaada huo wa fedha unaelekezwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) ili kutekeleza jukumu la usajili wa matukio muhimu ya Binadamu kwa ugatuzi (decentralization) kwa Watoto wenyewe umri chini ya mkaa mitano wapatao 152,546 ambaao watasajiliwa na kupatiwa yeti vya kuzaliwa katika wilaya 11 za mkoa wa Tanga.

Mkataba huo umesainiwa leo Juni 23, 2023 Jijini Dar es salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Nattu Mwamba na Balozi wa Italia Mhe. Marco Lombardi hapa nchini Mhe. Marco Lombardi.

"Tunaishukuru serikali ya Italia



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Nattu Mwamba na Balozi wa Italia Mhe. Marco Lombardi wakisaini Mkataba wa kuipatia Tanzania msaada wa fedha ili kuimarisha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu.

kwa ushirikiano katika kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi,

chi, tunawaahidi fedha zilitolewa zitafanya kazi ili-yokusudiwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Katiba na Sheria na

Wizara ya Fedha na Mpango". Alisema Dkt. Mwamba.

Msaada huo utahusisha Kitengo cha Usajili, Unuvi, Masoko Mawa siliano na Elimu kwa Umama, kitengo cha TEHAMA na kitengo cha Mipango na Ufuatiliaji.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Nattu Mwamba na Balozi wa Italia Mhe. Marco Lombardi wakikabidhiana mkataba mara baada ya kusainiwa katika hafla iliyofanyika Jijini Dar es salaam.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri RITA Dkt. Amina Msengwa akitoa neno la shukrani kwa Serikali ya Tanzania na Italia kusaini Mkataba utakaosa idia kuboresha hali ya usajili wa vizazi hapa nchini hususani katika Mkoa wa Tanga.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA Dkt. Amina Msengwa (wakwanza kushoto) akifuatiwa na Kabidhi Wasii Mkuu Bw. Frank Kanyusi na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu Bi. Irene Leslie wakifuatilia utajji saini mkataba baina ya Tanzania na Italia.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Nattu Mwamba akiwasilisha akiishukuru Serikali ya Italia kwa kuendelea kusaidia jamii katika kuboresha huduma mbalimbali za kijamii hapa nchini.



Balozi wa Italia Mhe. Marco Lombardi akieleza ushirikiano uliopo katika masuala ya uchumi, na maendeleo ya Jamii na kuahidi huwa Serikali yake itaendelea kudumisha ushirikiano uliopo.

### Picha ya kumbukumbu



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Nattu Mwamba na Balozi wa Italia Mhe. Marco Lombardi wakiwa katika picha ya kumbukumbu na baadhi ya ujumbe kutoka Serikali ya Tanzania na Italia mara baada ya kusainiwa kwa mkataba husika.



ritatanzania



ritatanzania1

PIGA BURE **0800117482**